



**SIMBA
CEMENT**
STRENGTH WITHIN

TAARIFA KWA WANAHISA TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

(Imeshirikishwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba mkutano Mkuu wa Mwaka wa ishiringi na sita wa wanahisa wa Tanga Cement Public Limited Company utafanyika kwa njia ya mtandao wa Microsoft Teams, siku ya Ijumaa tarehe 28 Agosti 2020 kuanzia saa nne kamili (4.00) asubuhi. Kampuni itawafahamisha wanahisa jinsi ya kujiunga na kushiriki kupitia namba zao za simu zilizosajiliwa na pia zipo kwenye kumbukumbu. Madhumuni ya mkutano ni yafuatayo:

1. Taarifa ya Mkutano

Taarifa ya kuitisha mkutano ichukuliwe kama inavyosomeka.

2. Kupitisha Kumbukumbu

Kuidhinisha na kusaini kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka wa ishiringi na tano uliofanyika tarehe 23 Agosti 2019.

3. Taarifa za Fedha na Ripoti za Wakurugenzi

Kupitia na kupitisha Taarifa za Fedha na ripoti za Wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2019.

4. Gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2019

Wanahisa kuzingatia pendekezo kutoka Bodi ya wakurugenzi la kutotangaza gawio la mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2019.

5. Uteuzi wa Wakurugenzi

Kuteua Wakurugenzi wa Bodi.

6. Kuidhinisha Mapato ya Wakurugenzi

Kuidhinisha mapato ya wakurugenzi kwa mwaka wa fedha 2020.

7. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje

Kuidhinisha uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa mwaka wa fedha 2020.

8. Mengineyo

Mwanachama yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi ambaye atapiga kupiga kura kwa niaba yake. Kama mwanachama ni shirika basi anatakiwa kuwasilisha fomu za uwakilishi pamoja na maamuzi ya Bodi ya kuthibitisha uteuzi wake kama mwakilishi wao. Fomu hizo zifike katika ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni si chini ya saa 48 kabla ya muda wa mkutano kuanza. Wanachama au wawakilishi wanatakiwa kuja na risiti inayothibitisha kuwa wamepokea fomu ya uwakilishi, kopi za fomu ya uwakilishi na kitambulisho kwaajili ya usajili.

Kwa agizo la Bodi.

Quresh Ganijee
Katibu wa Kampuni
28 Julai 2020